
# Kristo 8



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


ACHA NIKUELEZE HADITHI.
MTU MMOJA ALIKUWA NA MTINI KWENYE SHAMBA LA MIZABIBU.
KILA ALIPOIANGALIA KUTAFUTA MATUNDA HAKUPATA.
AKAMWAMBIA MTUNZAJI SHAMBA, "MIAKA MITATU SIJAPATA MATUNDA KWENYE MTI HUU!"
AKAMWAMURU, "UKATE CHINI! KWA NINI UHARIBU HATA ARDHI?"
MTUNZAJI SHAMBA AKASEMA, "BWANA, UACHE HATA MWAKA HUU.
"NIUPALILIE NA NIULTILIE SAMADI.
"UKIZAA MATUNDA MWAKA UJAO, SAWA!
"USIPOZAA, BASI TUTAUKATA."
LUKA 13:6-8


BAADAYE KWENYE SABATO YESU ALIFUNZA KWENYE SINAGOGI.
...UFALME WA MBINGUNI NI KAMA--
NGOJA. YULE MSICHANA PALE...
NIMEKUWA HIVI MIAKA KUMI NA MINANE.
NIMEKUJA KUPONYWA...
MSICHANA.
U HURU--
--KUTOKA KUTESEKA HUKU!
NI NINI HII?
TULIPEWA SIKU SITA KUFANYA KAZI!
INAFAA UJE KUPONYWA SIKU HIZO!
SIO SABATO!



LUKA 13:10-14



NYINYI WANAFIKI!
JE MNAFUNGUA PUNDA WENU KUNYWA MAJI SIKU YA SABATO?
KWA HIYO MSICHANA HUYU, MWANA WA IBRAHIMU NA SARA, KAMA NYINYI--
--ASIWEKWE HURU KUTOKA MATESO HAYA ALIYOFUNGWA NA SHETANI KWA MIAKA KUMI NA MINANE?
UFALME WA MBINGUNI NI KAMA MBEGU YA HARADALI!
ILIKUWA MTI NDIO NDEGE WATUE!
AU KAMA HAMIRA! WEKA KIWANGO KIDOGO KWENYE UNGA MWINGI--
NA BADO YACHANGANYIKA-NA NA UNGA WOTE.


LUKA 13:15-20






YOHANA 10:22-38


--NISIPOFANYA ANACHOKIFANYA BABA YANGU.
LAKINI NAFANYA!
AMINI MIUJIZA HATA MSIPOYAAMINI MANENO!
MUELEWE BABA YUPO NDANI YANGU!
NA NI NDANI YA BABA!
MSHIKE!
MSHIKENI!
MPELEKENI NJE YA JIJI MUMPIGE MAWE!
NIMEANZA KUELEWA ULICHOMAANISHA ULIPOSEMA--
--"IJAPO WAANGALIA HAWAONI, IJAPO WASIKIZA HAWASIKII WALA KUELEWA."
YESU ALIRUDI YORDANI YOHANA ALIPOBATIZA WATU.
YOHANA HAKUTENDA MIUJIZA--
--LAKINI KILA ALICHOKISEMA KUMHUSU HUYU YESU NI UKWELI!
YOHANA 10:38-42


ALIENDELEA KUFUNZA HUKU AKIENDA KWENYE MIJI NA VIJIJI.
BWANA, WATU WANGAPI WATAOKOLEWA?
WACHACHE TU?
WAWEZA KUWA WAWANIA KUINGIA MLANGO MWEMBAMBA.
SABABU WENGI WATAINGIA LAKINI MWENYEWE AKIFUNGA MLANGO?
MTAWACHWA NJE MKIBISHA MKIOMBA AWAFUNGULIE!
ATAJIBU, "SIWAJUI."
MTASEMA, "TULIKATA MKATE NAWE NA UKATUFUNZA!"
NA ATASEMA, "SIWAJUA NYIE! ONDOKENI WATENDA UOVU!"
YAFAA UONDOKE MWENYEWE!
ONDOKA!
TUACHE KWA AMANI!
HERODE ATAKA KUKUUA!
MWAWEZA KUMUAMBIA MBWEHA YULE NITAFUKUZA MAPEPO NA KUPONYA WAGONJWA--
--NA SIKU YA TATU NITALIFIKIA LENGO LANGU.
LAKINI MSITIE SHAKA HAPA!
MANABII HAWAWEZI KUFA NJE YA YERUSALEMU!
YERSUALEMU.
WAWAPIGA MAWE WALIOTUMWA KWAKO.
NILITAMANI KUWALETA CHINI YA BAWA LANGU KAMA KUKU AFANYAVYO KUWALINDA VIFARANGA.
LAKINI HAMUKUTAKA.


NYUMBA YA YERUSALEMU ITAJAWA NA UKIWA.
NA WEWE EH YERUSALEMU HUTANIONA TENA HADI USEMAPO, "HERI NI ANAYEKUJA KWA JINA LA BWANA."
RABI KESHO NI SABATO.
UTAITUNUKU NYUMBA YANGU KWA KULA NASI?
NDIO RAFIKI YANGU.
SABATO...
NIAMBIENI KAMA WATAALAM WA SHERIA--
--NI HALALI KUPONYA SIKU YA SABATO?


WAFANYA NINI?
KARIBU.
ASANTE!
KAMA MWANAO AU HATA NG'OMBE WAKO ANGEANGUKA KISIMANI SIKU YA SABATO UNGEFANYA NINI?
HAPA NI NYUMBANI KWANGU.
SAMAHANI.
WENZANGU WENGINE WASHAKAA KWENYE KICHWA CHA MEZA.
NAELEWA.
FUNZO!
USIKAE KWENYE KITI CHA MHESHIMIWA UALIKWAPO KWENYE KARAMU!
MAANAKE UTAAIBIKA--



LUKA 14:1-11


--MWENYE NYUMBA ATAKAPOKUSOGEZA KWENYE KITI CHA YAKHE.
UKICHUKUA NAFASI YA CHINI MWENYE NYUMBA ATAKAA PAHALI PA KUHESHIMIWA.
JIINUE USHUSHWE!
JISHUSHE UINULIWE.
NA MSIWAALIKE TU MARAFIKI NA JAMAA NA MAJIRANI MATAJIRI KWENYE SHEREHE ZENU!
KWA NINI?
WANAWEZA KUKUALIKA NA UTALIPWA.
BADALA YAKE WAALIKE MASKINI NA VILEMA NA VIPOFU NA VIWETE.
UTABARIKIWA!
SI NAO LAKINI KWENYE KUFUFUKA KWA WENYE HAKI!
HERI NI YULE NAYEKULA KWENYE SHEREHE KATIKA UFALME WA MUNGU!
MTU FLANI ALITAYARISHA SHEREHE KUU AKAWAALIKA WAGENI WENGI.
LAKINI ILIPOKUWA TAYARI WALIOALOKWA WALITOA SABABU WASIJE.
MTU YULE ALIKASIRIKA!
ALIMUAMBIWA MFANYAKAZI WAKE AENDE NJIANI NA KWENYE VICHOCHORO AWALETE MASKINI NNA VIWETE!
ALISEMA, "ENDA BARABARANI NA VIJIJINI! NATAKA NYUMBA YANGU IJAE!"
"ILA NILIOWAALIKA MBELENI HAWATAWAHI KUONJA KARAMU YANGU!"

LUKA 14:9-24






LUKA 14:25-15:2



WAPUMBAVU!
HAMUELEWI!
FIKIRIA UNA KONDOO MIA NA MMOJA ATOROKE!
UTAACHA WALE TISINI NA TISA UMTAFUTE YULE MMOJA, SIO?
MWANAMKE ALIYEKUWA NA SHILINGI KUMI ZA FEDHA AKIPOTEZA MOJA ATATAFUTA KILA MAHALI!
AKIIPATA ATASHEREHEKEA NA KILA MMOJA!
VIVYO HIVYO MALAIKA MBINGUNI HUFURAHIA MWENYE DHAMBI MMOJA AKITUBU!


LUKA 15:1-10


FIKIRIA BABA NA WANA WAWILI.
MWANA MMOJA AULIZA KIPANDE CHAKE CHA URITHI.
KWA HIYO BABA AKAGAWA KILA KITU.
"MWANA YULE ALIMUACHA BABAKE."
"ALIBADHIRI MALI KWA MAISHA YA ANASA!"
"HELA ZAKE ZILIPOISHA NJAA KUU ILITOKEA."
"HAKUWA NA CHOCHOTE WALE YEYOTE."
"LAZI YA KUWALISHA NGURUWE HAIKUTOSHA KUMLISHA."
"ALIGUNDUA WAFANYIKAZI WA BABAKE WALIANGALIWA VIZURI ZAIDI."
"ALIPORUDI BABAKE ALIMKIMBILIA NA KUMKUMBATIA!"
"ALIAGIZA SHEREHE KUMTUNUKU MWANAWE KWA SABABU:"
MWANAGU ALIPOTEA HIVI SASA KAPATIKANA!
"FIKIRIA KUSHEREHEKEA!
LUKA 15:11-27


YULE MWANA MWENGINE--
--ALIYEKUWA KABAKI NA BABAKE--
--ALIKUA SHAMBANI MDOGO WAKE ALIPORUDI.
"KIJANA MKUBWA ALISHIKWA NA HASIRA!"
"ALIKATAA KUINGIA NDANI."
"BABA YAO ALITOKA NJE KUMSIHI."
NILIKAA NAWE NIKAKUTII!
HUKUNIPA LOLOTE! ALIHARIBU KILA ULICHOMPA!
NA SASA WAMUANDALIA SHEREHE?
ULIKUA NA UTAKUA NAMI.
KILA NINACHO NI CHAKO.
HUWEZI KUSHEREHEKEA KUWA NDUGUYO ALIYETUACHA AMERUDI?
LUKA 15:25-32


SIKIZA. YEYOTE ALIYE MUAMINIFU NA KIDOGO ATAAMINIKA NA KINGI.
ALIYE MKORA NA KIDOGO SANA ATAKUA MKORA NA KINGI PIA.
USIPOKUWA MKWELI NA MALI ZA DUNIA, NANI ATAKAYEKUAMINI NA MALI ZA KWELI?
HAKUNA ANAYEWEZA KUWAFANYIA MABWANA WAWILI.
HUWEZI KUABUDU MUNGU NA PESA.
MUNGU AIJUA MIOYO YENU.
MWAJIFANYA WAZURI KWA WANAADAM.
LAKINI MUNGU ANACHUKIA VITU MNAVYOVITHAMI-NI.
ACHA NIKUAMBIE HADITHI NYENGINE MOJA.
TAJIRI ALIKUA NA MASKINI ANAYEOMBA LANGONI MWAKE.



LUKA 16:1-19



"MASKINI ALIITWA LAZARO."
"ALITAMANI KULA HATA CHENGA KUTOKA MEZANI MWA TAJIRI."
"LAZARO ALIKUFA."
"PIA TAJIRI NAYE."
"MASKINI ALIBEBWA HADI KWA IBRAHIMU."
"TAJIRI ALITESWA JEHANAM."
TAFADHALI! MTUME LAZARO AKIINGIZE KIDOLE CHAKE KWENYE MAJI NA AGUSE TU ULIMI WANGU!
MAISHANI MWAKO ULIKUA NA VITU VIZURI!
LAZARO ALIPOKEA VITU VIBAYA TU!
SASA LAZARO ALIWAZWA NA WAUMIA!
BASI MTUME LAZARO KWA NDUGU ZANGU!
ACHA AWATAHADHIRISHE DHIDI YA TESO HILI LA KUTISHA!
MWANYA HUU HAUPITIKI!


LUKA 16:20-27






LUKA 16:29-17:10



KWNEYE NJIA KATI YA SAMARIA NA GALILAYA...
YESU! BWANA!
TUONEE IMANI.
TAFADHALI.
ENDA.
JIONYESHENI KWA MAKUHANI.
NI MUUJIZA!
NAWEZA KUHISI VIDONDA VYANGU VIKIFUNGIKA!
AMETENDA, VILE TULIVYOAMBIWA ANAWEZA!
MMOJA MWENYE UKOMA AKASIMAMA...
AMETENDA...
MUNGU ASIFIWE!!!
BWANA! BWANA! ASANTE!
NILIPONYA KUMI!
WENGINE WAKO WAPI?
MMOJA TU NDIYE ALIREGEA KUMPA MUNGU SHUKRANI - NA MGENI!
INUKA UENDE - IMANI YAKO IMEKUPONYA.


BAADAYE...
MWALIMU!
TUNA SWALI KWAKO KAMA UNA MDA!
NINAO.
TUMESOMA MAANDIKO KWA MIAKA.
NA TUMEZINGATIA HISTORIA NA MATUKIO YA SASA.
KITU KIMOJA BADO HATUNA HAKIKA.
UFALME WA MUNGU UTAKUJA LINI?
UCHUNGUZI WENU WOTE NA HAMUELEWI, SIO?
WATU HAWATAWEZA KUSEMA, "NDIO HUU, UFALME WA MUNGU UMEFIKA!"
KWA SABABU UFALME WA MUNGU U NDANI YENU!
KARIBUNI MTATAMANI KUIONA SIKU YA MWANA WA ADAMU.
NA WENGINE WATASEMA, "WAKATI NI SASA!" MSIWAFUATE WATU HAO!
KWA WAKATI WA MWANADAM KUTAKUA KAMA UMEME
ONA INAVYOWAKA NA KUANGAZA ANGA!
ITAKUWA KAMA SIKU ZA NUHU!
WATU WALIISHI MAISHA YAO: WALIKULA, WAKAOA, WAKAFANYA KAZI.
KISHA MAFURIKO YAKAJA NA KILA KITU KILIHARIBIWA!



LUKA 17:20-27


SAWA NA SIKU ZA LUTU!
WATU WALINUNUA NA KUUZA, KUPANDA NA KUJENGA!
LAKINI LUTU ALIPOONDO-KA--
--MOTO NA SULFURI ULINYESHA CHINI TOKA MBINGUNI, VIKIHARIBU KILA KITU!
NI KAMA ITAKAVYOKUWA SIKU YA MWANA WA ADAM
KAMA UKO KWENYE PAA AU SHAMBANI SIKU HIYO IKIFIKA--
--USIRUDI NYUMBANI KWAKO KUCHUKUA CHOCHOTE!
"MNAKUMBUKA MKE WA LUTU?"
"WALIAMRISHWA KUONDOKA WALA WASITAZAME NYUMA LAKINI HAKUFANYA WALIVYOAMBIWA."
"ALIGEUZWA CHUMVI."
"UKIIPONYA NAFSI YAKO, UTAIANGAMIZA."
"NI KWA KUYAPOTEZA MAISHA YAKO NDIO UTAYADUMISHA."
SIKU HIYO WAWILI WATAKUWA KITANDANI NA MMOJA ATACHUKULIWA.
WANAWAKE WAWILI WATASAGA NAFAKA PAMOJA, MMOJA ATACHUKULIWA.
LAKINI KABLA SIKU HIYO MWANA WA ADAMU LAZIMA ATESEKE KWENYE MIKONO YA KIZAZI HIKI.


CHOCHOTE KITAKACHOJIRI INAFAA UOMBE WALA USIKATE TAMAA.
FIKIRIA HAKIMU ASIYEJALI MUNGU AU WANAADAMU!
KILA SIKU MWANAMKE ALIKUJA KWAKE AKIULIZA HAKI DHIDI YA MTU ALIYEMKOSEA!
HATIMAYE ALIJIBU OMBI LAKE!
KWA NINI? KWA KUWA ALIKUWA MWENYE HAKI? LA! MAANAKE AMEUDHIKA NAYE!
LAKINI UNAMUOMBA MUNGU MWENYE HAKI NA ANAYEKUPENDA.
TUZUNGUMZIE MAOMBI RAFIKI ZANGU.
MFARISAYO NA MTOZA USHURU WALIENDA KUOMBA HEKALUNI SIKU MMOJA.
MFARISAYO ALIPIGA KELELE HIVI!
"MUNGU NAKUSHUKURU SIKO KAMA MTOZA USHURU HUYU."
"NAFUNGA MARA MBILI KWA JUMA NA KUTOA FUNGU LA KUMI KWA MAPATO YANGU YOTE!"
MTOZA USHURU?
HAKUTHUBUTU HATA KUANGALIA JUU, ALIOMBA--
"MUNGU NIONEE HURUMA MIMI MWENYE DHAMBI."
NI NANI ALIYEENDA AMESAMEHEWA MBELE ZA MUNGU?
NAWAAMBIENI ANAYEJISHUSHA ATAINULIWA.
ANTAYEJIINUA ATASHUSHWA.




YOHANA 11:1-16





YOHANA 11:17-33


YUKO WAPI?
NJOO UONE, BWANA.
TWENDE.
HIVI, BWANA.
AWAJALI SANA!
YASIKITISHA HAKUFIKA MAPEMA!
APONYA WATU SAA ZOTE NA ANGEMPONYA LAZARO!
YUKO PALE, YESU...






YOHANA 11:39-43





YOHANA 11:44


TWAJARIBU KUFANYA NINI?
UMESKIA KILICHOJIRI?
AMEFUFUA MTU TOKA MAUTI!
WATU WAMFAUATA! WAMUAMINI!
WARUMI HAWATAFURAHI!
WATU WAKIMFUATA MTU HUYU, ITATUGHARIMU NINI?
WARUMI WATACHUKUA KILA TUNACHO!
HATUWEZI KUWA NA UASI!
WAPUMBAVU!
HAMJUI LOLOTE!
SI HERI MTU MMOJA AFE KWA NIABA YA WATU KULIKO NCHI NZIMA KUANGAMIA?
KAMA KUHANI MKUU MWAKA HUO, KAYAFA ALITABIRI KUMHUSU YESU.
ATAKUFA.
SIO TU KWETU SISI LAKINI KWA WANA WOTE WALIOTAWAN-YIKA WA MUNGU.
TUTAUNGAN-ISHWA TENA
KISHA TUJUE TUTACHOFAN-YA.
SWALI LILILOKO NI VIPI...
NA WAKAPANGA KUYACHUKUA MAISHA YAKE.



JOHN 11:45-54


NILIKUWEKO DADA ZANGU WALIPOMKARIBISHA YESU NYUMBANI KWETU.
HADITHI YA NDUGU ALIYEKUFA
"NJOO MBELE"
BWANA!
MWAMBIE MARIA ANISAIDIE!
KWANI HUJALI KUWA YUKO HAPO NDANI AKINIACHA NIFANYE KAZI YOTE PEKE YANGU?
MARTA UNA WASIWASI NA KUKASIRISHWA NA MAMBO MENGI MADOGO.
KITU KIMOJA TU CHASTAHILI WASIWASI...
NA MIMI KAMA DADA ZANGU NIKAWA MMOJA WA WANAFUNZI WAKE.
NISIWE? KUKIKUWA NA NGUVU KWENYE MAFUNDISHO NA ISHARA ZAKE.
LAKINI SIO KILA MMOJA ALIFURAHIKIA MAFUNZO YAKE NA ISHARA.
ILIBIDI AONDOKE ENEO HILO WAKATI TISHIO KWENYE MAISHA YAKE LILISEMEKANA.
KISHA MDA BAADA YA YEYE KUONDOKA...
AH... HAPANA...
UCHUNGU MWINGI AJABU.
LAZARO, WANISIKIA?
TUTAFANYAJE?
NILIDHOOFIKA UCHUNGU ULIPOENDEAL KUZIDI.


KULIKO UCHUNGU WA KIMWILI--
KAMA YESU ANGEKUWA HAPA WAJUA ANGEWAPONYA!
LAKINI HAYUKO!
NA WALA HATUJASIKIA LOLOTE TOKA KWAKE!
--UCHUNGU MWINGI WALIOHISI KWA SABABU YANGU.
LAZARO?
NINI INAENDELEA?
SIKUWA NA UWEZO WA KUFANYA LOLOTE KUWALIWAZA.
WATULIZE.
TUMECHELEWA!
MBONA YESU HAKUJA?
HAPANA! JAMANI, HAPANA!!!
AMEKWENDA...
YAMEISHA.
KISHA HATIMAYE KWA REHEMA UCHUNGU UKADIDIMIA.
PIA SAUTI NA RANGI NA WOGA UKADIDIMIA PIA.
MPAKA KULIPOKUWA NA--
--HAMNA?
HAPANA.


SIO ETI HAMNA LAKINI HAKUNA NACHOKIKUMBUKA.
SAA ZENGINE NASKIA AU KUHISI KITU KINACHOLETA KUMBUKUMBU.
LAKINI NI KUMBUKUMBU AMBAYO HATA NINGEIKUMBUKA SIDHANI NINGEIELEWA.
LAKINI BAADA YA MDA NISIOUJUA KITU KILINIVUTA NYUMA.
KITU AMBACHO SITAKISAHAU.
SAUTI.
LAZARO!
TOKA NJE!
NA VYOTE VILIVYODIDIMIA VIKARUDI.
NILIHISI KITU KIKIUFINIKA USO WANGU, KUNIKOSESHA PUMZI.


GIZA LIKAGEUKA MWANGAZA.
SI MWANGA MKUU ILA KARIBU UYAPOFUSHE MACHO YANGU.
HARUFU ILIINGIA PUANI MWANGU PUMZI IKAJAA MAPAFUNI.
OOOAFF!
HIYO... HARUFU...
MISULI ILINIUMA NA KUKAZANA.
LAKINI UCHUNGU WA UGONJWA WANGU ULIPOTEA.
SIKUJUA KILICHOKUWA CHAFANYIKA KWANGU.
SIKUJUA NILIVYOFIKA PALE.
SIKUJUA KWA NINI NILIKUWA PALE.
NILIJUA KITU KIMOJA TU.
NILISIKIA AMRI.
NA AMRI HIYO LAZIMA KUITII.


"MAZISHI...
NGUO..."?
TOA HIZO
NGUO MAITI!


BAADAYE NILIIISIKIA HADITHI.
YESU ALIVYOFIKA BAADA YA MIMI KUZIKWA.
MADADA ZANGU WALIVYOSEMA ALICHELEWA.
NA ALIVYODHIHIRISHA HAKUWA TU NA UWEZO WA KUPONYA.
ALIKUWA NA NGUVU JUU YA UHAI NA KIFO.
KWA HIYO, SIKUSHANGAA KUPATA YANGU SI JENEZA TUPU YESU ALILOLIACHA NYUMA.
SASA NASEMA HADITHI YANGU KWA KILA ATAKAYENISIKIZA.
ALILIITA JINA LANGU NA KUNIPA MAISHA MAPYA.
NA ANALIITA JINA LAKO NA ATAKUPA MAISHA MAPYA PIA.
HICHO NDIO KITU KIMOJA KINACHOSTAHILI WASI WASI...

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."





# SUPERBIBLE.TV